Tanzania kuuza nyama Saudi Arabia

>>Uk.5

Prof. Kabudi awahimiza vijana kupigania nchi yao

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Profesa Palamagamba Kabudi, amewataka vijana wote nchini kuona fahari ya kuzaliwa Tanzania, hivyo wapambane...

>>Uk.5

UHURU

ISSN 0876 - 3896 Na. 24082 Jumatatu Agosti 9, 2021 Tanzania sh 1,000

Ukweli Daima

@Uhuruonline Website: uhurumedia.co.tz

Wanakiji wachoma gari la halmashauri

>>Uk.9

1, 008,400| Idadi ya dozi za chanjo zilizosambazwa mikoa yote 26

Serikali yaonya matumizi vyeti 'feki' vya chanjo

> **Yasema** watakaokamatwa wakivitumia watachukuliwa hatua za kisheria

>**Watu** 105, 745 wameshachanjwa, 164, 500 wamejiandikisha

>**Ufuatiliaji** kwa waliochanjwa unafanyika kupitia vituo vya afya, waganga wakuu >>Uk.2

Serikali inatoa tahadhari iwapo kuna watu watakaojaribu kujipatia vyeti vya chanjo kwa njia ya udanganyifu, watakaoinika na mfumo na kuchukuliwa hatua za kisheria. Natoa wito kwa watoa huduma ya chanjo, kila mmoja kutimiza wajibu wake na kujiepusha na udanganyifu wowote.

PROFESA MAKUBI

JENEZA lenye mwili wa aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Elias Kwandikwa, likishushwa na na maofisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), kutoka kwenye helikopta ya jeshi, baada ya kuwasili kijijini kwake, Bulike, Kata ya Kinamapula, Halmashauri ya Ushetu, mkoani Shinyanga, jana.

Picha na Anthony Mhengenu

Bei mpya ya mbaazi, kunde yawapandisha mzuka wakulima

>>Uk.3

Shaka ataja siri CCM kukubalika

>**Asema** kutojitambua kwa vyama vya upinzani, viongozi wake kutoandaliwa katika misingi imara ni miongoni mwa sababu

>**Atoa** somo kwa wapinzani kuacha kudandia hoja kwa kufuata mkumbo akisema ni miongoni mwa mambo yanayowadumaza

>>Uk.3

Scanned with CamScanner

Mitandao @JAMVILAHABARI Jamvi la habari jamvihabari +255676807684 Email: jamvilahabari@gmail.com

JAMVI LA HABARI

GAZETI LAKO

ISSN/Toleo Na. 2683-6548 Toleo Na. 1455 JUMATATU AGOSTI 09, 2021 Bei Tsh. 1000 Kenya Ksh. 60 www.jamvilahabari.co.tz

MAPOKEO CHANYA CHANJO YA CORONA

- Hadi kufikia Agosti 4, 2021 dozi 1,008,400 chanjo zimesambazwa katika mikoa yote 26 na vituo zaidi ya 550
- Kufiki Agosti 7,2021 zaidi ya watu 169,500 waliweka 'Booking' ili kupatiwa chanjo, huku wengine 105,745 wakiwa tayari wameshapatiwa chanjo
- Kwa sasa serikali inajipanga kutoa vyeti vya kidijitali (Covid 19 Vaccine Electronic Certificates) hata kwa wale waliochanjwa na kupatiwa vyeti vya karatasi

UK. 4

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan, akiwasili katika Uwanja wa Ndege [illegible] 2021 [illegible] Dar es Salaam [illegible]

Tanzania kuuza nyama nchini Saudi Arabia

UK. 4



Wananchi waitaka serikali kufanya operesheni ya kuwasaka wanaotupa watoto

UK. 5

Scanned with CamScanner

Tanzania kuuza nyama Saudi Arabia

Na Mbaraka Kambona

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante ole Gabriel amekutana na ujumbe wa Saudi Arabia kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara ya nyama na nchi hiyo.

Profesa Gabriel alikutana juzi Dar es Salaam, na ujumbe huo ulioongozwa na Mkaguzi wa Mamlaka ya Dawa na Chakula wa Saudi Arabia, Ahmed Alhajouj.

Kwa mujibu wa Profesa Gabriel kabla ya kukutana nao, ujumbe huo ulikagua maeneo yanayohusika na uchakataji mazao ya mifugo yakiwamo machinjio, maabara na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na kujiridhisha na kutoa mapendekezo kadhaa ya kuboresha, ili biashara hiyo ifanyike kwa viwango vinavyohitajika na nchi hiyo.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameielekeza Wizara kutafuta masoko nje ya nchi, hivyo inaendelea na jitihada ikiwemo hatua hiyo ya kutafuta soko Saudi Arabia.

"Haya masoko ya nje ya nchi ni mazuri, kwa sababu yanatupa fedha za kigeni, lakini pia yanawahakikishia wafugaji soko la uhakika kwa mazao ya mifugo yao," alisema Profesa Gabriel.

Aidha, alitoa rai kwa wafugaji kuchukulia hatua hiyo kama fursa kubwa kwao, na hivyo wahakikishe wanaboresha ufugaji wao kuwa wa kisasa zaidi, ili kukidhi soko hilo la kimataifa.

"Serikali ni rahisi kutafuta masoko, lakini je, mifugo iliyopo inakidhi soko hilo? Niwaombe wafugaji na wafanyabiashara watumie fursa hii vizuri ili kuboresha uchumi wao na wa Taifa pia," aliongeza Profesa Gabriel.

Alisema Sekta ya Mifugo kwa sasa inachangia pato la Taifa kwa asilimia 7.4 lakini lengo la Wizara ni kufikia asilimia 15 ifikapo mwaka 2025, na hilo linawezekana kama milango ya masoko nje ya nchi ikianza kufunguka kwa uhakika.

Msajili wa Bodi ya Nyama, Dk Daniel Mushi aliishukuru Serikali kwa jitihada inazofanya kwa kushirikiana na wadau kufungua masoko mengine nje ya nchi, ili kuuza nyama katika masoko yanayolipa bei nzuri.

Hivi karibuni, Rais Samia alikutana na Mtoto wa Mfalme wa Saudi Arabia ambapo miongoni mwa maeneo yaliyoangaliwa, ni pamoja na Sekta ya Mifugo na aliielekeza Wizara kutafuta masoko nje ya nchi ikiwamo Saudi Arabia.



Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante ole Gabriel (katikati) akiwa na ujumbe wa Saudi Arabia jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto kwake ni Mkaguzi wa Mamlaka ya Dawa na Chakula wa Saudi Arabia, Ahmed Alhajouj. (Na Mpiga Picha Maalumu).

Matumizi potofu gesi chanzo cha majanga

Na Gift Mathias, Moshi

MATUMIZI yasiyo sahihi ya nishati ya gesi za majumbani yametajwa kuwa chanzo kinachochangia majanga ya moto katika jamii ikiwa ni pamoja na kuteketea kwa nyumba na kusababisha vifo.

Kwa hali hiyo, jitihada za utoaji elimu zimeendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na Jeshi la Zimamoto ambapo kimsingi vipo vifaa vya kuzima moto, ambavyo hupatikana kwa ujazo na viwango tofauti.

Alisema ni vyema kwenye taasisi na majumbani, vikawapo vifaa hivyo ambapo kwa siku hizi vipo ambavyo hugundua dalili za moto na kutoa ishara kabla ya moto kutokea, hivyo kuzuia madhara.

"Kuna vifaa vya aina nyingi ambavyo ukivifunga nyumbani au kwenye jengo

Miti 8,500,000 k mikoa ya Kanda

Na Nashon Kennedy, Mwanza

JUMLA ya miti 8,500,000 inatarajiwa kupandwa kwa ukanda wa mikoa ya Kanda ya Ziwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/22 kwa ajili ya kutunza mazingira, kuongeza lishe na kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Kamishina Msaidizi wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Ebrantino Mgie alisema hayo jana jijini Mwanza wakati akitoa taarifa kwa Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya TFS.

Alisema miche ya miti hiyo ambayo imezalishwa na TFS itapandwa katika kila halmashauri, taasisi za umma na kwa wananchi.

Mgie alisema kwa halmashauri za Misungwi, Musoma, Bariadi na Geita jumla ya miti 1,000,000 itapandwa, Nyamagana na Silayo-1500,000, Rubare na Buhindi-1,300,000 na miti 500,000 itapandwa katika shule za msingi na sekondari na 900,000 kwenye halmashauri za Bukoba na Chato.

Katibu Tawala Mkoa wa Mwanza, Ngusa Samike akizungumza na ujumbe huo ofisini kwake, aliipongeza TFS kwa jitihada zake za kuzalisha miti ya mbao na matunda na k
inapandwa ka
mengi nchini.

Aliitaka Bo
ya TFS iweke
ka kupanda n
ya asili hasa k
ya kwenye mi

"Binafsi n
kufanya hama
na halmashau



Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel (katikati) akizungumza na ujumbe kutoka Saudi Arabia ukiongozwa na Mkaguzi wa Mamlaka ya Dawa na Chakula, Ahmed Alhajouj (kushoto) alipokutana nao Dar es Salaam juzi. (Na Mpigapicha Wetu)

M
m

Na
Sur

N
wa
wa
Dk
Kas
ame
um
wa
kati
una
ia m
za u
mko
hum

Scanned with CamScanner

FURSA KIMATAIFA

Tanzania kuanza kuuza nyama Saudi Arabia

Mwandishi Wetu, Mwananchi

Dar es Salaam. Ujumbe kutoka nchini Saudi Arabia ukiongozwa na mkaguzi wa Mamlaka ya Dawa na Chakula nchini humo, Ahmed Alhajouj umekagua maeneo yanayohusika na uchakataji wa mazao ya mifugo yakiwamo machinjio, maabara na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili Tanzania ianze kupeleka nyama nchini humo.

Licha ya ukaguzi huo, ujumbe huo pia umetoa mapendekezo ya kuboresha ili nyama itakayosafirishwa ikidhi vigezo na viwango vinavyohitajika.

Akiupokea ujumbe huo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Ole Gabriel amesema wanatekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kutafuta masoko nje ya nchi ili kuongeza tija kwa wafugaji nchini.

"Masoko ya nje ni mazuri kwa sababu yanatupa fedha za kigeni na kuwahakikishia wafugaji soko la uhakika kwa mazao ya mifugo," alisema Profesa Gabriel.

'Ni rahisi Serikali kutafuta masoko lakini mifugo iliyopo inakidhi soko hilo? Niwaombe wafugaji na wfanyabiashara kutumia fursa hii vizuri ili kuboresha uchumi wao na wa Taifa.'

Profesa Gabriel

Katibu Mkuu wa Mifugo, Profesa Elisante Ole Gabriel (katikati) akizungumza na ujumbe kutoka nchini Saudi Arabia.

Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Dk Daniel Mushi alisema anaishukuru Serikali kwa kushirikiana na wadau kufungua masoko nje.

"Ujio wa ujumbe huo umetupa changamoto kwani kuna mambo tunapaswa kufanya ili nyama ya Tanzania iweze kukubalika. Ni lazima kuboresha lishe ya mifugo ili wanyama wakue kwa haraka wakiwa na nyama nyingi yenye ubora," alisema Dk Mushi.

Hivi karibuni Rais Samia alikutana na Mwanamfalme wa Saudi Arabia na kujadili masuala kadhaa.

Vijana wafundwa uchumi wa habari

Jesse Mikofu, Mwananchi

Unguja. Ili kushiriki vyema kukuza uchumi wa Taifa, vijana visiwani Zanzibar wamefundwa namna ya kuzichangamkia fursa zilizopo ndani ya uchumi wa bluu.

hamas ahiyo imetolewa kwenye kongamano la biashara na uchumi lilioandaliwa na Taasisi ya Mayoda Economic Development Group na kuyashirikisha makundi tofauti ya vijana.

Mchumi na mhadhiri mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Profesa Honest Ngowi uchumi wa bluu ni dhana mpya nchini lakini unazo fursa nyingi ukiwamo uvuvi na vifaa vyake, kilimo cha mwani, majogoo, ubaharia, boti, uchimbaji mafuta na gesi pamoja na usafirishaji.

"Idadi ya fursa ni kadri ya macho yako yanavyoona, hakuna fursa itakuafua ulipo badala yake wewe ndio unatakiwa kuzifuta zilipo," alisema Professa Ngowi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Mayoda Economic Development Group, Selemani Boko alisema: "Tunatamani kuona wazawa wanamiliki uchumi wa Taifa lao. Tumetengeneza programu tatu ikiwamo ya ubunifu wa mawazo yanayokusudia kutatua changamoto za jamii."

Mwenyekiti wa Umoja wa Makundi ya Vijana Zanzibar, Omar Simai Mmanga alisema wananchi wengi bado hawafahamu maana ya uchumi wa bluu hivyo elimu zaidi inahitajika hasa wa wananchi wlaiopo pembezoni mwa mji ili asiachwe yeyote kati yao.

2020

Mwaka ambao Rais Hussein Mwinyi alichaguliwa akiahidi kuimarisha uchumi.

05

Miaka ambayo Serikali ya Zanzibar imeahidi kuhamasisha uchumi wa bluu.

Scanned with CamScanner

Nipashe Uk.2

IFA



Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Prof. Elisante Ole Gabriel (katikati), akiongea na ujumbe kutoka nchini Saudi Arabia alipokutana nao jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Mkaguzi, Mamlaka ya Dawa na Chakula, Saudi Arabia, Ahmed Alhajouj. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

Scanned with CamScanner

Agosti 9,2021, Nipashe Uk.7

Serikali yaja na mikakati uboreshaji sekta ya uvuvi

Na Maulid Mmbaga

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), Dk. Rashid Tamatamah, amesema serikali imejipanga kwa kuweka mikakati ya kimaendeleo kwa miaka mitano, ambayo imetoa kipaumbele katika suala la uwekezaji.

Dk. Tamatamah aliiambia Nipashe kuwa maeneo makubwa ambayo yamelengwa katika uwekezaji ni uwekezaji wa uvuvi katika bahari kuu, ambao katika miaka mitano ijayo kwa upande wa bara serikali itanunua meli tano.

Alisema katika mwaka unaokuja, serikali itanunua meli tatu kati ya tano zilizopo ndani ya mpango, na zitakuwa zinaendeshwa na Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO) kwa kushirikiana na sekta binafsi.

"Sambamba na hilo uwekezaji mwingine mkubwa ambao serikali itaufanya ni ujenzi wa bandari ya uvuvi Bagamoyo, taratibu za maandalizi zimeshaanza, na tunategemea mwezi wa 10 tutaanza kutangaza zabuni ili ujenzi uanze," alisema.

Aliongeza kuwa kwa kuanzia, serikali imetenga shilingi bilioni 50 zitakazotumika kuanza ujenzi huo, na kwamba ujenzi huo utakuwa na manufaa mengi ikiwamo kuongeza kiwango cha uvuvi wa samaki.

Alisema faida nyingine ni kusaidia malighafi katika viwanda vya ndani pamoja na kusaidia wafanyabiashara kwa kupata samaki kwa bei nzuri.

"Eneo lingine la kuhakikisha tunaongeza uzalishaji wa samaki ni kupitia ufugaji au ukuzaji viumbe maji, watu wamehamasika katika ufugaji wa samaki... mwaka jana tulikuwa na wafugaji zaidi ya 20,000, na baada ya mwaka mmoja wameongezeka na kufikia 30,000," alisema.

Aidha, kila wanavyoongezeka watu ndipo mahitaji ya vifaranga vya samaki na chakula bora vinaongezeka, pia katika mwaka huu wanategemea uzalishaji utaongezeka kutoka tani 20,000 hadi tani 30,000, na kufikia mwaka 2030 wanategemea kufikia uzalishaji wa tani 100,000 za samaki.

Scanned with CamScanner